HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA

Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa,
Idara ya Maendeleo ya Jamii.
S.L.P. 28,
SHINYANGA.

13/02/2017

Mhe, Mwenyekiti
Kamati ya Fedha na Utawala
HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA

YAH: MAPENDEKEZO YA TARATIBU ZA UTOAJI MIKOPO KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE NA VIJANA MANISPAA YA SHINYANGA.

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake na Vijana ulianzishwa na Serikali mnamo mwaka 1993/94, ikiwa ni utekelezaji wa azimio la Bunge kwa mujibu wa Sheria, chini ya kifungu namba 17 (1) cha "**The exchequer and Audit ordinance (cap. 439) No. 21 of 1961**".

2.0 LENGO NA MADHUMUNI YA MFUKO

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Lengo na Madhumuni ya mfuko huu ni;

- Kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake na vijana wenye kipato kidogo ili kuwawezesha kujiendeleza kiuchumi na hivyo kuinua hali ya familia zao na kukuza uchumi wa Nchi.
- Kuwa kama mfuko wa dhamana
- Kuongeza ajira na kipato kwa wanawake na vijana katika sekta isiyo rasmi.
- Kujenga tabia ya kujiwekea akiba kwa ajili ya upanuzi wa shughuli zao na dharura.
- Kutafuta vyanzo vya fedha.

3.0 WALENGWA WA MFUKO HUU

Mheshimiwa Mwenyekiti

Walengwa wa Mfuko ni;

- Wanawake wenye umri wa miaka 18 na kuendelea, na walio chini ya umri huo ambao wana watoto.
- Vijana wenye umri wa kuanzia miaka kumi na mitano (15) hadi thelathini na tano (35) tu.

Scanned by CamScanner

4.0 MIONGOZO YA WIZARA KATIKA KUTOA MIKOPO

Utaratibu wa Wizara kuhusu utoaji wa mikopo kwa vikundi vya Wanawake na Vijana ni huu ufuatao;

a) **Wanawake:**

- Halmashauri inapaswa kuhakikisha kwamba mikopo inatolewa kwa shughuli yoyote halali za uzalishaji kama vile kilimo cha mazao ya biashara na chakula, ufugaji, uvuvi biashara n,k,
- Maombi ya mikopo ya mwanakikundi yaambatishwe na mchanganuo wa mradi wa mwanakikundi na kuwasilishwa kwenye kikundi na yajadiliwe kwa kina katika mikutano ya kikundi au chama kabla ya kuchukua fomu.
- Fomu za maombi zitolewe na Afisa Maendeleo ya Jamii (Jinsia) na fomu hizo ziwe na namba.
- Wanakikundi wajidhamini, mwanakikundi mmoja adhaminiwe na wenzake wanne.
- Fomu ya maombi iwasilishwe na uongozi wa kikundi kwa Afisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya kata.
- Mratibu wa Mfuko athibitishe kuwepo kwa kikundi au chama cha kuweka na kukopa kwa kuwasiliana na uongozi wa sehemu husika.
- Maombi hayo yaidhinishwe na Afisa anayesimamia Mfuko ngazi ya kata (CDO).
- Kamati ya Mikopo ya Halmashauri ijadili maombi yaliyowasilishwa kwa ajili ya kukubali au kukataa maombi hayo.
- Muda wa kupokea na kujadili fomu za maombi ya mikopo usizidi mwezi mmoja kabla ya kikundi kukubaliwa au kukataliwa.

Utaratibu wa kurejesha Mkopo

Ndugu Mwenyekiti,

Utaratibu wa marejesho uliopendekezwa na Wizara ni huu ufuatao;

- ❖ Marejesho ya kila mwezi
- ❖ Mkopaji arejeshe fedha kwa mweka Hazina wa Kikundi.
- ❖ Mweka Hazina apeleke fedha hizo benki kwenye akaunti ya mfuko na kuwasilisha ankara za benki kwa Afisa Maendeleo ya Jamii kata/Wilaya anayeshughulikia Mfuko na nakala kwa Mwenyekiti wa kikundi

a) **Vijana**

Utoaji mikopo kwa vikundi vya Vijana inapaswa kuzingatia yafuatayo:-

- Usajili wa kikundi
- Uhalisia wa Mradi.
- Upatikanaji wa soko.
- Utunzaji wa mazingira
- Uwezo wa kupunguza umaskini.
- Uelewa wa wanakikundi juu ya Mradi wenyewe

Scanned by CamScanner

- Uwezekano wa Mradi kulipa mkopo ndani ya miaka miwili
- Uwiano wa mkopo na mradi wenyewe.
- Ukamilifu wa nyaraka na viambatanisho.
- Kikundi kiwe na TIN namba na leseni
- Kikundi kiwe mwanachama wa SACCOs teule ya Vijana Manispaa.

5.0 TARATIBU ZA HALMASHAURI KATIKA KUTOA MIKOPO.

Mheshimiwa Mwenyekiti,
Kwa kuzingatia mwongozo wa uendeshaji wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF) wa Wizara ya Afya na Maendeleo ya Jamii Halmashauri imejiwekea taratibu zifuatazo hapo chini ambazo zilipitishwa na Baraza la Madiwani la Manispaa la tarehe 28/04/2015 Muht. BAR 05/2014/2015 AGD 5 na Kamati ya Fedha na Utawala tarehe 23/02/2015 Muht.F/A.10/2014/15 AGD.09 (uboreshaji wa taratibu za utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wajasiriamali Manispaa ya Shinyanga) ili kuboresha hali ya urejeshaji wa mikopo. Taratibu hizo ndizo zinazotumika kwa sasa.

Taratibu hizo ni hizi zifuatazo;

- Kutambuliwa na uongozi wa eneo mahali kikundi kilipo na kupitisha barua ya ombi la mkopo kwa Afisa Mtendaji wa Mtaa/Kijiji na Kata husika na kuwasilisha barua hiyo Idara ya Maendeleo ya Jamii Manispaa.
- Barua ya ombi la mkopo kuambatishwa na mchanganuo wa gharama za mradi/shughuli za uzalishaji mali ambazo zinaombewa fedha za mkopo.
- Kikundi kuwa hai (kinauwezo wa kujiendesha na kujiongoza).
- Kikundi kuwa na hati ya utambulisho na Katiba na kuitumia.
- Kikundi kuwa na uongozi na unaofanya kazi.
- Kikundi kiwe na Akaunti ya Benki NMB, tawi la Manonga Shinyanga, isiyopungua salio la Tsh 100,000/=
- Kila mwanakikundi kuwa na shughuli halali ya kiuchumi ambayo anauzoefu nayo.
- Kila mwanakikundi awe tayari kubeba deni la mwenzake ambaye ataacha kulipa kwa sababu yoyote ile.
- Wanakikundi kutafuta mdhamini atakayedhamini kikundi kwa dhamana isiyopungua thamani ya mkopo utakaotolewa. Mdhamini asiwe Diwani wala mtumishi wa Manispaa ya Shinyanga, kigezo hiki ni muhimu kizingatiwe ili kuhakikisha fedha za Halmashauri zinarejeshwa ipasavyo.
- Kila mwanakikundi kuwasilisha picha ndogo 1(passport size) kwa ajili ya kuzibandika kwenye jalada la kikundi.
- Afisa Mtendaji wa Kata kuwasilisha muhtasari wa WDC uliopitisha majina ya vikundi vilivyokamilisha taratibu zote tajwa hapo juu kwa Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa uhakiki zaidi.
- Kikundi kuhudhuria mafunzo ya ujasiamali/biashara kabla ya kupata mkopo.
- Kikundi kufunga mkataba wa miezi 10 na Halmashauri kuhusu urejeshaji wa mkopo.

Scanned by CamScanner